

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI-TAMISEMI
HALMASHAURI YA MJI BARIADI
SHULE YA SEKONDARI GUDUWI**

**S.L.P 97,
BARIADI.
TAREHE: 15/12/2020**

NDG. MZAZI/MLEZI WA _____

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI GUDUWI
KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari **GUDUWI** mwaka wa masomo 2021. Shule hii ni ya kutwa na mchanganyiko (Wasichana na Wavulana). Hongera sana.

Muhula wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021**. Hivyo, mwanao anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **07/01/2021** kwa ajili ya usajili na kuanza masomo. **MWISHO WA KURIPOTI NI TAREHE 13/01/2021, ENDAPO MWANAO HATAFIKA AU KUCHELEWA KUFIKA HATUA KALI ZA KISHERIA ZITACHUKULIWA DHIDI YAKO WEWE MZAZI/MLEZI.** Ni jukumu la mzazi/mlezi kuhakikisha kuwa mwanafunzi anawahi shuleni bila kukosa au kuchelewa baada ya kukamilisha mahitaji na taratibu zote zilizoелеkezwa katika barua hii.

MAHALI SHULE ILIPO:

Shule ipo Wilaya ya Bariadi, tarafa ya Ntuzu kata ya Guduwi katika Mtaa wa Guduwi.

MASOMO YANAYOFUNDISHWA SHULENI:

Atakapo kuwa hapa shuleni atapaswa kusoma masomo tisa 9 ambayo ni **CIVICS, HISTORY, GEOGRAPHY, ENGLISH LANGUAGE, KISWAHILI, PHYSICS, CHEMISTRY, BIOLOGY, BASIC MATHEMATICS**. Masomo yote yanafundishwa kwa lugha ya kingereza isipokuwa somo la kiswahili. Lugha ya mawasiliano shuleni ni kingereza tu.

MAHITAJI:

A. NDANI YA DARASA

1. Daftari 10 kubwa Quire 2, 3 au 4.
2. Mathematical Set 1 (Mkebe)
3. Kalamu za wino na penseli.
4. Begi la shule.
5. Kamusi ya Kiingereza – Kiingereza {Dictionary}

B. SARE YA SHULE:

1. **WAVULANA:**
 - Awe na shati mbili nyeupe mikono mifupi,
 - Tai mbili Kijani na Blue bahari,
 - Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kufungwa kwa kamba,
 - Soksi nyeupe jozi mbili,

- Suruali mbili rangi ya Blue bahari na Kijani (suruali iwe pana siyo chupa (Model) chini yenye turn-up, iwe na mifuko mitatu miwili mbele na mmoja nyuma),
- Mkanda wa Surulia wa ngozi mweusi na
- Sweta rangi ya blue.

2. **WASICHANA:**

- Awe na shati mbili mikono mifupi rangi nyeupe, shati liwe na mfuko mmoja mkono wa kushoto.
- Tai rangi ya Kijani na Blue bahari.
- Viatu vyeusi vya ngozi visigino vifupi.
- Soksi nyeupe jozi mbili.
- Sketi mbili rangi ya Kijani na Blue bahari, kitambaa kizito, sketi iwe **NDEFU** hadi kwenye kisigino
- Sweta rangi ya Blue.

NB: MAVAZI YASIYO YA HESHIMA HAYATAKIWI

3. **SARE YA MICHEZO:** Track suti ya Blue kwa Wasichana na T-shirt ya rangi ya Blue. Kwa Wavulana Bukta rangi ya Blue, Track suti Blue pamoja na raba za michezo jozi moja 1.

NB: T-SHIRT ZA SHULE RANGI NYEKUNDU ZENYE NEMBO ZA SHULE ZINAPATIKA SHULENI

Sare ya shule itavaliwa wakati wote mwanafunzi awapo shuleni, darasani, shughuli zote za kishule na wakati wa safari nje ya shule. Katika michezo kila mwanafunzi atatakiwa kuvaa sare ya michezo iliyoelekezwa katika fomu hii.

4. **VIFAA VYA USAFI:** Mwanafunzi anatakiwa kuja na ufagio wa nje (chelewa)

ANGALIZO

- Ni marufuku kwa mwanafunzi kuvaa viatu vya ghorofa (visigino virefu)
- Ni marufuku kwa mwanafunzi kuvaa nguo zisizo rasmi shuleni
- Ni marufuku kwa mwanafunzi kuvaa suruali mlegezo(kata K) na ukibainika hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yako
- Kila mwanafunzi anapaswa kuwa safi, kufanya usafi kikamilifu katika eneola shule alilopangiwa kila siku
- Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu kanuni, taratibu na sheria za shule. Hivyo, lazima awe na nidhamu ya hali ya juu.

C. MIPAKA YA SHULE

Kila mwanafunzi atatambulishwa mipaka ya shule na kuifahamu. Hivyo,

- (i) Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa nje ya eneo la shule katika muda anaotakiwa kuwepo shuleni bila ruhusa maalumu.
- (ii) Ni marufuku kutembelea sehemu zifuatazo hata kama sioi muda wa shule:-
 - Nyumba za kulala wageni(Guest house/Lodge)
 - Vilabu vya pombe(Bar)
 - Nyumba za walimu na Ofisi bila kibali
 - Kumbi za starehe

Pamoja na barua hii, nakufungashia fomu mbalimbali ambazo ni lazima zijazwe kikamilifu kabla ya kusajiliwa na msajili wa wanafunzi ha shuleni. Fomu hizo ni pamoja na sheria za shule, taarifa binafsi za mwanafunzi na vipimo vya daktari (Medical Examination Form) na uthibitisho wa mzazi/mlezi.

D. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE:

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebisha kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995 aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu Sayansi Teknolojia mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa na kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni

- (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote wa shule, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
- (c) Kushiriki kwa makini kufanya maanadalio ya jioni (Preparation)
- (d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote ukiwa kama mwanafunzi katika shule hii
- (f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
- (g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- (h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- (i) Kutunza mali za shule na za umma

E. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUSIMAMISHWA AU KUFUKUZWA SHULE:

- (a) Wizi
- (b) Uasherati na ushoga
- (c) Ubakaji
- (d) Kupiga au kupigana
- (e) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevywa kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi n.k
- (f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- (g) Kudharau Bendera ya Taifa
- (h) Kupata mimba au kumpa mtu mimba
- (i) Kuoja Kuolewa
- (j) Kutoa mimba
- (k) Kuwa na simu ya mkononi
- (l) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- (m) Kukataa adhabu kwa makusudi

KARIBU SANA GUDUWI SEKONDARI

SEIF MASOUD HAMAD
MKUU WA SHULE
0683 093 378 / 0753 919 928